# AFRI TWENDE

Kulitia moyo kanisa la Afrika katika kazi ya umisheni ulimwenguni

Jarida la 7, Toleo la 1
www.afrigo.org/afritwende



## KUMFIKIA MWISLAMU ALIYE JIRANI ULIMWENGUNI KOTE

- NINAWI YAMSUBIRI KILA MMOJA WETU
- KWA NINI TUWAFIKIE WAISLAMU
- TAYARI KWA UJENZI WA TAIFA

# YALIYOMO








## 04 WALIOITWA: TUMEAGIZWA KUHUBIRI HUKO AFRIKA YA KASKAZINI
Mmishenari kijana katika mazingira ya kazi yenye changamoto anatupa uzoefu wake.

## 05 NINAWI YAMSUBIRI KILA MKRISTO
Kijana wa miaka 20 anayehubiri Injili kwa Waislamu anaeleza mawazo yake juu ya akina Yona wa siku ya leo.

## 06 NENO AMBALO HALITARUDI BURE
Soma jinsi mvulana wa kisomalia alivyokua na kisha kuwa mmishenari miongoni mwa watu wake waliotawanyika ulimwenguni kote.

## 08 RASILIMALI KWA AJILI YA KUWAFIKIA WAISLAMU
Je unataka kuwafikia Waislam wanaokuzunguka lakini hujui namna ya kuanza? Timu ya AfriTwende imepata nyenzo au rasilimali zinazopatikana kwa urahisi kama vile mafunzo, vitabu na vyombo vya kunasia sauti (video) ili kukusaidia.

## 11 TAYARI KWA UJENZI WA TAIFA
Kutafuta msaada kwa ajili kuwatunza wamishenari inaweza kuwa ni kikwazo. Gundua jinsi mashirika mawili yanavyokabiliana na changamoto hii.

© 2024 AFRIGO
AfriTWENDE ni chapisho lenye lengo la kuleta ufahamu, uhamasishaji, mafunzo na kusajilisha kanisa na mtu mmoja mmoja katika Afrika kwa nia ya kujihusisha na umisheni duniani.

**Mhariri Mkuu:** Jesse Katabi Masolwa

**Msanifu:** Pilgrim Communications

**Picha kwenye jalada:** kwa hisani ya AIM Stories.

Maoni yaliyoelezwa katika makala za Gazeti hili siyo lazima yawe ya Mchapishaji.

Picha halisi hutumika inapobidi. Majina hutumika kwa sababu za kiusalama.



# KWA NINI TUWAFIKIE WAISLAMU?

NA RAY MENSAH

Hivi majuzi niliombwa kufundisha kozi juu ya 'Ukristo na Dini zingine za Ulimwengu' katika Taasisi moja ya kitheolojia. Nilipokuwa naandaa somo la kufundisha, nilibahatika kusoma makala iliyoandikwa na kiongozi wa huduma ambaye anawafikia Waislamu. Alikadiria kuwa asilimia 99 ya Wakristo hawajui namna ya kuwaeleza Injili watu wa imani zingine. Takwimu hizo za kushangaza zilinifanya nifikiri. Kitabu chenye taarifa za kikristo za Ulimwengu (Encyclopedia) kinaeleza kuwa asilimia 81 ya watu ambao si wakristo hawamjui mtu anayeitwa mfuasi wa Kristo. Nilikubali kuwa Kiongozi huyu wa Misheni anaweza kuwa hayuko mbali na ukweli.

Baadhi ya makanisa, mashirika ya umisheni, vituo vya mafunzo na wamishenari wanajifunza namna maalumu ya kuwafikia Waislamu, na kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Tunawapongeza sana wao pamoja na wainjilisti na wamishenari hawa wenye ujasiri.

Pia kuna kozi nzuri sana pamoja na vitabu vingi vizuri (angalia vitabu vingi vimetajwa kwenye ukurasa wa 8 & 9). Rasilimali hizi zinapaswa kupatikana kwa urahisi kwa mwili wa Kristo katika kuwawezesha mamilioni ya wafuasi wa Kristo kuwafikia Waislamu kikamilifu. Hili ni suala la haraka na ni wito unaotutaka tuchukue hatua.

Sababu kuu mbili kati ya nyingi za kwa nini Wakristo hawawafikii Waislamu na Injili ni hofu na upungufu wa maarifa juu ya namna bora ya kuwashuhudia habari za Injili. Mkristo wa kawaida anaweza kumshuhudia mkristo dhaifu habari za Kristo lakini atamruka mwislamu. Asilimia kubwa ya Wakristo wanafikiri wao na Waislamu wanaamini Mungu huyo huyo mmoja na kwa hiyo hawaoni hitaji la kuwahubiria Waislamu. Hali hii inatakiwa kusahihishwa na wachungaji wetu katika makanisa yetu.

Bwana wetu Yesu Kristo alisema wazi katika Mathayo 9:38 kuwa 'mavuno ni mengi lakini wavunaji ni wachache'. Mavuno haya ni pamoja na Waislamu. Mavuno ya Waislamu ni mengi lakini wavunaji wa kuwafikia ni wachache.

Kwa miaka mingi, kinyume na mitazamo ya watu, nimekuja kujua kuwa, Waislamu wengi wako wazi kwa Injili na wengi wao wako tayari kuu jua ukweli.

Tunahitajika kuomba kwa bidii ili BWANA wa mavuno ainue wamishenari kuwafikia Waislamu na wokovu kwa Waislamu ufike kote Afrika na ulimwenguni. Baadhi ya Waislamu wanakutana na Bwana Yesu kupitia ndoto na maono na wanaokoka kwa sababu mtu fulani aliwaeleza habari za Injili na aliwaombea kwa nguvu zake zote.

Kuna sababu kadhaa ambazo zinatufanya tuwafikie Waislamu; nitasema mbili tu. Ya kwanza, Kristo alilipa kanisa agizo kuu. Lazima tuwafanye mataifa kuwa wanafunzi wa Kristo (Mathayo 28:18-20), na ni lazima twende ulimwenguni kote kuhubiri Injili kwa kila mtu (Marko 16:5). Kwa hakika, kila mtu ikiwa ni pamoja na Waislamu.

Pili, Waislamu ni kundi kubwa la watu ambao bado hawajafikiwa katika ulimwengu. Kwa mujibu Kwa mujibu Joshua Project, kuna Waislamu wapatao bilioni 1.8 duniani kote na kuna makundi ya Waislamu yapatayo 3,467 ambayo bado hayajafikiwa na injili.

*Ray Mensa Mensah anatumika kama Mkurugenzi wa shirika linaloitwa 'One Way Africa' na ni Rais wa GEMA. Pia ni Mhariri wa Gazeti la Sauti ya Umisheni anayesimamia Shule ya Umisheni ya Jiwe Lililo hai. Unaweza kuwasiliana naye kwa: ray@owm.org*

# TUMEITWA TUMEAGIZWA KUHUBIRI INJILI KATIKA NCHI ZA AFRIKA YA KASKAZINI

Kufanya kazi katika Afrika Kaskazini inaweza kuwa ni hatari, na Daudi anajua hili vizuri. Polisi humfuata Daudi anakoenda; wakiwa na wasiwasi na uwepo wa Wakristo. Baadhi ya majirani zake humkejeli na hata wamekuwa wakimtishia kifo.

“Hapo mwanzoni ilikuwa ngumu sana, lakini sasa najua kuwa huwa nachunguzwa. Nimeishi kwa miaka minne kwa namna hii.” Hata hivyo, Daudi ana uhakika kwa kiasi fulani kuwa hata akikamatwa hatapigwa, lakini anaweza kufukuzwa nchini.

Uhakika wake kuwa jina la Kristo lazima lijulikane na ndiyo ujumbe uliomleta hapo.‘ Nilipokuja kwa Yesu, kumjua yeye ilikuwa moja ya vitu vikubwa nilivyovipata, lakini nilijifunza kuwa kuna mahali pengine ambapo hakuna makanisa kabisa na kwa hivyo hakuna mtu wa kuwaeleza habari za Injili.’ Daudi alitafuta mitandao kama vile ile ya Mradi wa Yoshua ili kujifunza zaidi. ‘Mungu alianza kugusa moyo wangu’ anasema Daudi.

Hatimaye, alihudhuria mafunzo ya umisheni na kuanza kutumika miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya huko Kaskazini, ambapo ni makanisa machache tu yanapatikana tena katika miji mikubwa tu lakini hakuna makanisa kwenye maeneo mengi. Daudi alibarikiwa kufanya kazi kwa muda na mmishenari mmoja na kushirikiana na makanisa ya wenyeji. Mahali anapoishi Daudi sasa, vijana wanataka kujua zaidi.

Polisi wanachunguza kanisa dogo na kuona ni nani huwa anakuja



na kuondoka. Wakati mwingine wanaangalia vitambulisho vya wale wanaohudhuria kanisani. Polisi wanaweza kuwapa taarifa zao na wanaweza hata kupoteza kazi zao na hata marafiki. Wanafamilia ya mwamini mpya wanaweza kumpiga au hata kumkataa kabisa.

Kwa ujumla, Daudi anakutana kwa siri na wale ambao wanapenda kusikia habari za Yesu, ingawa hii bado ni hatari kwake. Aliwahi kukutana na mtu ambaye alionekana ana hamu ya kusikia habari za Yesu, lakini mtu huyo baadaye alimtumia ujumbe wenye vitisho vya kifo.

Kuwa mtu mweusi ni changamoto nyingine pia. ‘Kwa nyakati fulani husema mambo ya kibaguzi dhidi yangu. Ni vigumu hata kwenda madukani. Unapotaka kupanga nyumba, mwenyeji atakubali wakati mnaongea naye kwenye simu lakini ukienda kumwona anakukatalia.

Hata hivyo hali hiyo ni tofauti kwa wakristo. Daudi anaweza kukaa kwenye nyumba za wakristo kwa muda. Katika ushirika na wakristo, humtia moyo Daudi na hivyo kumpunguzia magumu ya maisha.

Tuliongea na Daudi muda mfupi kabla ya noeli, na kwa kweli alikuwa anasubiri kwa kusanyiko la wakristo kutoka sehemu zote za nchi siku hiyo ya noeli.

Alipoulizwa kama anajisikia vizuri kuwa na familia, Daudi alicheka. “Baadhi ya wanawake katika kanisa langu la nyumbani wanasema hawawezi kuja hapa.” Akaendelea kusema, ‘ Lakini kama Mungu anamwita mmoja wao, basi tunaweza kuwa na familia hapa. Kuna changamoto, lakini kwa Mungu kila kitu kinawezekana.”

Ushauri wa Daudi kwa kijana mwenye wito kwa ajili ya watu ambao bado hawajafikiwa uko dhahiri : “Nakushauri kuwa na kanisa linalokutuma. Hii ni muhimu sana.” Anasema kwamba anapoenda nyumbani, kanisa lake humpa muda wa kutoa ushuhuda, na kisha kumwombea na kumsaidia. Anapopata changamoto, viongozi humpa ushauri. Huu ni msaada wa thamani.

‘Vijana wengi wanataka kufanikiwa kufanya kitu kwa ajili ya Mungu, lakini wachache wanafahamu kwamba tunaishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Vijana wana hisia kuwa umisheni ni kazi nzuri, lakini umisheni ni kazi ya pole pole na ngumu. Daudi anavumilia na anaona matunda.



# NINAWI YAMSUBIRI KILA MKRISTO

NA JARED OGINGA

Umeshawahi kufikiria kwa nini Yona alipata misukosuko yote ya kwenda kuwaonya wakazi wa Ninawi juu ya hukumu, katika mji ambao ulikuwa na wakazi 120,000 tu? Leo inakadiriwa kuwa kuna Waislamu wapata o bilioni 1.8 ulimwenguni kote, ambapo kati yao milioni 446 wanaishi katika bara la Afrika pekee. Mungu anawapenda hawa Waislamu pia, lakini bado hawajamjua na kuonja pendo lake. Mkristo wa kawaida ana ufahamu mdogo sana juu ya Uislamu na Mwislamu. Watu wengi wanawaogopa Waislamu kutokana na hali tete ya asili katika uhusiano kati ya Wakristo na Waislamu. Hata hivyo, wengi wa Waislamu hufurahia mazungumzo au mijadala ya kidini pamoja na Wakristo. Pengine, kama ilivyokuwa kwa Waninawi, Waislamu wako huru kuzungumza kuhusu masuala ya kidini kuliko tunavyofikria.

## Kwa nini Tuwafikie Waislamu?

Kwa ujumla, watu wanafikiri kuwa ni vigumu kwa Mwislamu kuja kwa Kristo. Lakini hii si ndivyo ilikuwa hata kwetu kabla ya kuokoka? Ugumu huu kwa kiasi fulani unatokana na asili ya dini yenyewe ya Kiislamu, ambayo hufanya kazi kwa mfumo kama vile chanjo. Uislamu ni dini ambayo humpa Mwislamu nusu ukweli kuhusu Mungu, ili anapokutana na ukweli halisi basi akili zake huusukumia mbali au kuujua ukweli. Inahitajika juhudi kuweza kuvunja kizuizi hiki.

Habari ya Yona hunisisimua. Yona alipotumwa kwenda Ninawi, si tu kwamba hakuwa tayari bali alikimbilia kwenda upande mwingine. Leo baadhi ya makanisa na waumini wanakaidi uharaka huu wa kazi ya kuwafikia Waislamu wakati wengine wakiu kimbia kabisa wajibu huu.

> Watu wanafikiri kuwa ni vigumu kwa Mwislamu kuja Kristo. Lakini hii si ndivyo ilikuwa hata kwetu kabla ya kuokoka?

Kama ambavyo BWANA alituma samaki mkubwa kwenda kummeza Yona, tunajua anaweza kuziba njia za watumishi wake kuukimbia wito.

Leo kundi kubwa la watu ambao bado hawajafikiwa ni la wale ambao hujitambulisha kama Waislamu, ambao kama Kristo angerudi leo hatima yao ingekuwa ni kuishi mbali na Kristo.

## Je, kanisa linajali kuhusu kuwafikia Waislamu kama inavyotakiwa?

Nilijiunga na shirika la Life Challenge Afrika nikitokea chuoni, kama mratibu wa mahusiano watu. Siku moja nilizuru moja ya makanisa makubwa katika Jiji la Nairobi kukuza na kuhamasisha kijitabu cha siku 30 za maombi kwa Waislamu. Mchungaji Mwandamizi alikuwa akikagua ujenzi hapo kanisani kwake. Nilimweleza kwa nini kanisa linahitajika kujihusisha na Waislamu na hata kuwekeza pesa ili kupata vitabu vya maombi- ili kuwaombea Waislamu wakati wa mwezi wa Ramadhani.

Mchungaji alinisikiliza kwa makini. Baada ya kumaliza, alinionyesha kwenye kona ya eneo la ujenzi na kusema kwa upole, "kijana [nilikuwa kijana mdogo wakati huo] unavi ona vile vyoo? Tunahitaji kumaliza hivyo kwanza. Rasilimali zetu zote za pesa tumezielekeza kwenye mradi huo."

Nilihuzunika, lakini niliweka kusudio kutembelea tena kanisa hilo. Leo, kanisa hilo siyo tu linaomba kama mwanzoni nilivyoomba bali ni moja ya makusanyiko ambayo yanaelekeza rasilimali watu na pesa kuwafikia Waislamu katika Kenya na nje ya Kenya.

Kwa nini kanisa liwajali Waislamu? Swali hili lina majibu mawili. Kwanza, kusudi la msingi kwa kanisa ni kumfanya Kristo kujulikana kwa wale ambao bado hawajasikia Injili (Matendo 1: 8). Kwa hiyo, kanisa lipo kwa ajili ya wasioamini. Kama kanisa haliwafikii wale walioko nje ya kuta zake basi hapo tunamwangusha Bwana Yesu.

Pili, Waislamu ni sehemu kubwa ya watu ambao hawajafikiwa kabisa. Ili kanisa la Afrika lionekane kweli linashughulika na umisheni, ni lazima liwafikie Waislamu.

Kuwafikia Waislamu kunahitaji mafunzo ya msingi katika kuujua Uislamu, kujua kuitetea imani ya kiKristo na kuwa na njia za matendo.

## Kanisa Lianzie Wapi?

Kwa kuanzia, kanisa linapaswa kumuhamasisha kila mkristo; huduma ya injili kwa Waislamu haijahifadhiwa kwa ajili ya watu wachache tu. Mwitikio wa kwanza ni kufanya maombi kwa bidii. Pili, kanisa lazima litenge rasilimali fedha ili wale wenye shauku ya kuwafikia Waislamu waweze kupata mafunzo na kuandaliwa kwa kazi hiyo.

Kwa vile tunamtumikia Mungu mwenye upendo, anayejali na kutamani watu wote wapate maarifa ya kumjua Kristo anayeokoa, sisi tulioitwa kwa jina lake hatuna uchaguzi bali kuwapenda Waislamu kikweli kweli, kuwaombea kila mara, na kuteka kila fursa kuwashirikisha habari za Kristo kwa njia ya ufasaha.

*Jared Oginga ni makamu Mkurugenzi wa Shirika la Life Change Afrika ambapo amelitumikia kwa miaka 22 sasa. Mtembelea kupitia: https://life-challenge.org/ Barua pepe: Jared.oginga@sim.org.*



# NENO
## AMBALO HALITARUDI BURE

Akiwa na umri wa miaka 12, mvulana wa kisomali, alikuwa tayari alishajifunza Kurani yote. Aliweka kwenye kumbukumbu sehemu za Kurani kwa Kiarabu, lugha ambayo hata alikuwa hajui maana yake. Alipofikia umri wa miaka 18, alikwenda kuishi na mjomba wake katika Jiji la Mogadishu. Siku moja alikuta kitabu kwenye kabati la kuwekea vitabu, chenye jina ‘ Bibilia Takatifu.’ Akifikria kuwa ni Koran iliyotafsiriwa kwa Kisomali, alianza kuisoma. Katika hali ya mshangao, aligundua kuwa kitabu hicho cha Biblia, kilikuwa kinahusu imani tofauti na kwamba mjomba wake alikuwa mfuasi wa Yesu Kristo. Alimwomba Allah amsamehe kwa kugusa na ‘kitabu cha makafiri.’ Lakini kitu fulani kilimvuta.


Picha na AIM Stories

"Niliendelea kukisoma," anasema. "Nilihisi kuwa hili lilikuwa ndilo Neno la Mungu lililokamilika na la kwanza. Kadiri nilivyosoma Agano Jipya, haiba na ujumbe wa Yesu Kristo viligusa moyo wangu. Kama mwislamu, namwabudu Allah kwa njia ya kuogopa, lakini kupitia kwa Yesu, Mungu ni baba yangu ambaye ananipenda zaidi ya anavyonipenda baba yangu mzazi."

Baada ya miaka miwili ya usomaji wa Biblia, Mungu alimwondolea hofu zote na Abdi alimwamini Yesu kwa ukamilifu wote kama ‘njia, kweli na uzima’ (Yohana 14:6).


Picha na AIM Stories

Hatimaye, alipata ujasiri wa kumwomba mjomba wake kwenda naye kanisani. Alijiunga na ushirika mdogo la kiprotestanti wa watu kama 20 hivi katika mji wa Mogadishu, ambapo alifundishwa kuwa mwanafunzi na kubatizwa mwaka 1989.

Miaka 30 baadaye Abdi Duale na mke wake Kawser Omar ni wamishenari wanaofanya kazi pamoja na SIM, wakiwafikia Wasomali kwa injili duniani kote, wakitumia njia mbalimbali kupitia majukwaa ya mtandaoni.

### KUTAZAMA NYUMA


Kuna usemi kwamba, "kuwa msomali ni kuwa mwislamu." Uislamu ulifika karne ya 8 nchini Somalia, na leo hii wasomali karibu wote wanaishi maisha ya Uislamu wa Sunni. Misheni za Kikristo zilianza kwenye miaka ya 1880 lakini zilikumbana na changamoto nyingi. Biblia nzima inapatikana kwa lugha ya kisomali, lakini ni asilimia chini ya moja tu ya wasomali wote ni wakristo. Wasomali wameridhika na Uislamu na wanaona unajitosheleza, huku wakipinga na kutumia nguvu ya upinzani wa kijamii kwa wale wanaothubutu kumfuata Kristo.

Vita vya wao kwa wao nchini Somalia vilivyo anza mwaka 1987 hadi 1991 na viliifanya Somalia itangazwe kuwa ni "nchi iliyoanguka kiutawala." Wakristo wengi waliuawa, ikiwa ni pamoja na mjomba wake Abdi. Sehemu ya Somalia iliyojulikana kama Somaliland ilijimega na kujitenga na hivyo kwa sehemu kubwa imebaki na amani wakati Somalia imeendelea kuteseka kwa vurugu na njaa. Theluthi moja ya nchi inadhibitiwa na kundi la kigaidi la Al-shabaab. Vita pia imefanya Wasomalia wengi kuikimbia nchi na kwenda uhamishoni katika sehemu mbalimbali za dunia.

### VYOMBO VYA HABARI VYA MAISHA MAPYA

Kama ambavyo Abdi aliweza kupata kitabu kwenye shelfu ya vitabu vya mjomba wake, huduma ya vyombo vya habari vya maisha mapya inatoa fursa kwa wasomali kutafuta Biblia pale wanapongalia tovuti na mitandao ya kijamii.

Huduma hii ilianza mwaka 1972 kama sauti ya matangazo ya Redio ya masafa mafupi ya Maisha Mapya na




iliendelea kupanuka na mwaka 2006 ilianza kupatikana kwenye tovuti na mwaka 2014 ilianza kupatikana kwenye Facebook na YouTube. Majukwaa haya huwapa watu nafasi kujua ukweli wa Mungu wakiwa kwenye usiri majumbani kwao. Kwa hiyo, Wakristo wanaweza kufanya ushuhudiaji kwa ujasiri bila hatari inayoweza kutokana na kuhubiri injili hadharani.

Maudhui ya mtandaoni yanajumuisha aina nyingi za Biblia, pamoja na viwezeshi vya kompyuta kama URLS, zinazomsaidia msomaji kutafuta sura na mistari ya Biblia kwa urahisi. Miziki ya Kikristo kwa Kisomali pia inawekwa kwenye mitandao hii ya kijamii. Video ya hivi karibuni mtandaoni ya wimbo kuhusu mateso wa *Kan ii dudayaa yeelkii* (Sijali juu ya yule anayeniudhi) ilipata watazamaji zaidi 210,000.

Mfuatano wa video unaoitwa Neno la Mungu na methali za kisomali zilizowekwa kwenye mtandao hivi karibuni ambayo ilikuwa na hoja zinazopinga mtazamo kuwa ni vigumu kubadilika, ilitazamwa na watu zaidi ya milioni moja. Mjumuiko wa hadhira ni wa juu, na lengo la maudhui ni kufikia mawasiliano ya uso kwa uso pamoja kwa minajili ya kujifunza zaidi.

Abdi anasema kwamba kwa wale wanaomfuata Yesu, wengi wao inawachukua miaka mingi kuweza kumwambia mtu kuhusu habari za Yesu, wakiweza. Anaongeza Abdi, " wamekuwa mateka wa utamaduni.' Abdi na mkewe Kawser wanakabiliwa na vitisho ambavyo Abdi anaviita kuwa ni vya "kawaida". Haya yanakuja kama maoni kupitia video zinazowekwa kwenye mitandao ya kijamii. Familia yao imepuuza vitisho hivyo tangu walipogeukia imani ya kiKristo miongo kadhaa iliyopita.

## RUNINGA YA INJILI YA SOMALIA

Mwaka 2020 Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, aliitisha siku ya kitaifa ya maombi. Abdi na mkewe Kawser walialikwa kuwasilisha kipindi kwa lugha ya kisomali ambacho kilirushwa kwenye Runinga ya kitaifa inayoonekana nchini kote Mei 10, 2020. Kipindi cha pili cha ibada kilirushwa mwezi Juni 2021. Mkurugenzi wa New Life Media, Michael Madany, alisema, " Kwa kadiri tunavyojua, hii ni mara ya kwanza kwa kipindi cha kikristo katika lugha ya kisomali kutangazwa na runinga ya taifa.'" Kwa kadiri tunavyojua, hii ni mara ya kwanza kwa kipindi cha kikristo katika lugha ya kisomali kutangazwa na runinga ya taifa."

Tangu wakati huo, kupitia ushirika na shirika la kimisheni la SIM, na la Kuhubiri Injili katika pembe ya Afrika (The Horn of Africa Evangelical Mission), vipindi zaidi vimeandaliwa kwa ajili ya kutangazwa kupitia runinga ya Setelaiti ya shirika la Uinjilisti la Ethiopia. Ni kupitia njia hii ndipo Runinga ya Injili ya kisomali ilizaliwa mwaka 2021.

Pamoja na vikwazo vikubwa vya kiasili dhidi ya uinjilisti na upandaji wa makanisa miongoni mwa wasomali, njia mpya za kidijitali zinabeba neno lililo hai la Mungu kwenda kwenye nyumba na mioyo ya watu ambao BWANA wetu hajawasahau. Washuhudiaji waaminifu kama Abdi, mkewe Kawser na timu yao wanahatarisha maisha kwa kuamini kuwa Neno litatimiza kile ambacho Mungu anapendezwa nacho na litafanikiwa kwa kile lililotumwa kufanya (Isaya 55:11).

**TAFADHALI OMBA KWA AJILI YA:**

- Kwa Wakristo waweze kuomba na kuwafikia Wasomali walio nje ya nchi yao.
- Ulinzi kwa waumini na wafanyakazi wa huduma.
- Maarifa ya kupambanua roho wanapokutana na ngome za giza.
- Kumshukuru Mungu kwa ajili ya watu wanaojifunza kupitia mitandao na watenda kazi wa huduma ya Mungu Mmoja, Njia Moja.
- Wote wanaohusika na kazi hiyo.

## JIFUNZE ZAIDI

- Somali worship service on Ethiopian TV: https://bit.ly/Somaliworship
- Somali Gospel TV - Facebook: https://bit.ly/3NJ31C5
- Somali Gospel TV - YouTube: https://bit.ly/3NMwBXa
- New Life website: https://noloshacusub.com/

## Ushuhuda wa Msomali

"Nawasalimu katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kupitia yeye nimepata wokovu, neema na uzima wa milele. Kwangu kuwa mkristo kumeniletea shida nyingi. Mke wangu na watoto wetu watano walianiacha pale niliposema siwezi kuikana imani yangu katika Kristo. Nilihukumiwa kwenda jela kwa miezi 20, lakini niliachiliwa baada ya miezi sita tu. Hakuna mtu aliyenifanya mimi kuwa mkristo; hiyo ilikuwa ni kazi ya Mungu. Sijawahi kumwona mkristo mwingine; hata hivyo, nimepakua Biblia ya kisomali kwenye simu yangu. Sijasoma sana, na nafanya kazi kama kibarua. Nimekuwa mkristo kwa miaka sita sasa na bado ni mchanga katika kutumia mitandao ya kijamii kama Facebook. Simu yangu ya mkononi ya kwanza ilikuwa ndogo sana; angalau ilikuwa na Google na kwa hiyo niliweza kupakua Biblia. Nimeisoma karibu yote kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Namshukuru BWANA ambaye alinikomboa kutoka gizani, kwenye ujinga na kivuli cha mauti. Natembelea kila tovuti ya kisomali inayotangaza Injili ya Mungu."

# UNAWEZA KUWAFIKIA WAISLAMU:

Je unataka kuwafikia Waislamu wanaokuzunguka, lakini unaanzaje? Timu ya AfriTWENDE imetayarisha vitabu, kozi, na video vya kukusaidia.

**Shirika la Life Challenge Afrika (LCA)** lina aina mbalimbali za vitabu kwenye tovuti yao. Vingi vya vitabu hivi vinapatikana kama PDFs na bei zake ni ndogo. LCA ina PDFs za mada za aina mbalimbali ambazo zinaweza kukusaidia kufahamu Uislamu na Waislamu.

https://www.life-challenge.org/resources/


LCA imeturuhusu kwa uzuri kabisa kutumia baadhi ya rasilimali zao kwenye kurasa ya tovuti yetu, ili uweze kupakua bila malipo. Tembelea uone kilichopo kutoka AfriTWENDE.

https://afrigo.org/islam-resources-swahili/

## VITABU:


### Mambo yaliyosabisha Maendeleo ya Uislamu

Kipeperushi hiki kinaongelea pale Uislamu kikielezea kwa kifupi chimbuko, muanzilishi na kwa namna ipi Uislamu uliendelezwa. Lakini pia kinaelezea uislamu na baadhi ya maneno muhimu na maana zake katika dini hii.





### Nani Anakwenda Mbinguni

Huu ni ushuhuda mfupi wa Isaka kuhusiana na mtu aliyesahihi kwenda mbinguni na atakaye kwenda jehanamu. umegusia safari yake ya familia ya uislamu mpaka pale alipompokea Kristo na maisha yake akiwa anamtumikia Mungu.




### Uislamu na Waislamu

Kitabu kinaeleza kuhusiana na Uislamu, amri zake, Kurani, na vitu vya kujua kama mkristo kwenye Kurani, uislam ulipoanzia, Mwanzo wa maisha ya mtume Muhamadi kwa undani zaidi kuanzia kuzaliwa kwake, maisha aliyoishi hadi mwisho, pamoja na imani yao juu ya Allah. Lakini pia inaeleza namna tunavyoweza kulinganisha ile Kweli ya Yesu kwa Busara kama mkristo kutokana na Kurani hoja ambazo Waislamu wanajenga kutokana na ukristo na injili na mengineyo mengi kiundani zaidi.




### Mambo Kurani hufundisha kuhusu Biblia

Kitabu hiki kinakupa muangaza kwa kifupi vile Kurani hufundisha waumini wake juu ya Biblia na namna wanavyoitafsiri Biblia. Vitabu hiki kinakupa muangaza kwa kifupi vile Kurani hufundisha waumini wake juu ya Biblia na namna wanavyoitafsiri Biblia.





### Habari zako Unazijua

Kitabu hiki kidogo kinaongelea namna habari za mwanadamu zimeanzaa katika msingi mkuu wa Mungu na kuishia na Mungu kuanzia kwenye kuzaliwa na imani ya mwanadamu laana na ahadi ya Mungu kwake hata baada ya kuasi, na sadaka aliyoitoa Mungu kupitia mwana wake pale msalabani. Kama vile maandiko matakatifu yalivyo nukuliwa na kutunzwa bila ya hivyo hakuna ambaye angeweza kujua habari zake na historia yake bila ya Mungu.





### Umeumbwa kwa Kusudi

Kitabu hiki kinafafanua kusudi la kuumbwa kwako, na safari ya mwanadamu kwa ujumla tangu alipoumbwa na Mungu, ahadi aliyopewa na Mungu, alipoanguka na Msamaha wa milele aliopewa na Mungu.



# RASILIMALI ZA KUKUSAIDIA




## SHIRIKI HII

Mtu Mwenye Ujumbe wa kijitabu hiki kinaweza kupakuliwa bila malipo kwenye tovuti yetu ya https://afrigo.org/islam-resources-swahili/ na kinaweza sambazwa kwa marafiki waislamu, majirani na wanafamilia. Itumie ikiwa ni zana ya uinjilisti.


Picha na AIM Stories

## KUWASHUHUDIA WAISLAMU KWA HEKIMA

By Jared Oginga, Life Challenge Africa

1. **Hofu na Ujinga:** Tafuta kuujua Uislamu kama mfumo, na Waislamu kama watu waliopendwa na Mungu, lakini wamenaswa kwenye mtego wa mfumo wa dini. Ujinga na hofu kutoka kwa Wakristo ndivyo vinavyozuia kazi ya kuwashuhudia Waislamu. Mwislamu atafahamu Injili kwa kiwango kile ambacho wewe unafahamu imani yako na yeye kama mtu.
2. **Jenga mahusiano ya kweli na upendo wa kweli na Waislamu (Warumi 2:9):** Uinjilisti kwa Waislamu kimsingi umejikita kwenye kujenga mahusiano ya kweli na urafiki. Jitahidi kufahamu kazi yake, familia yake, marafiki n.k., na fanya hivyo kwa undani kabisa. Jaribu kujua hofu zake, furaha, na mapambano yake ya maisha ya kila siku na matumaini yake. Uhusiano wa namna hii unatakiwa utokane na upendo, ili ajisikie upendo wa Kristo ndani yake.
3. **Jenga kuaminiana:** Wakristo siyo binadamu bora kupita binadamui wote; tuna upungufu wetu kama binadamu. Mweleze rafiki yako Mwislamu ukweli na jinsi neema ya Mungu inavyokusaidia wewe kuishi maisha ya kikristo.
4. **Inachukua Muda:** Kila kitu unachomwambia mwislamu analinganisha na alichofundishwa kwenye dini yake. Ujumbe wa Injili siyo tu unatakiwa kuonekana ni wa maana kwa Mwislamu bali unatakiwa umfanye kuona hitaji la kuupokea tofauti na alichonacho.
5. **Usipuuze maswali yake:** Kweli zote za kibiblia lazima zielezwe vizuri na kueleweka; kusiwe na ukweli wenye ubabaishaji. Kuacha imani yake na kuwa mkristo ni uamuzi mgumu ambao muiislam anaweza kuufanya katika maisha yake, na katika hili atataka kuwa na uhakika wa uamuzi wake.
6. **Nenda naye pole pole hatua kwa hatua:** Hisia zake na hofu siyo tu kwamba ni za kidini; nyingine ni za kibinafsi. Anahitaji uhakika, mwongozo na pia usaidizi.
7. **Makabiliano au makaribisho?** Injili ni kinyume na kile ambacho Uislamu unamuahidi mwanadamu, na kwa hiyo kutakuwa na maeneo ya kutofautiana. Usikwepe maswali magumu. Jaribu kujibu maswali yote kibiblia kwa kadiri unavyoweza. Kama huna jibu la kibiblia, usivumbue la kwako. Uwe mkweli. Hakuna mkristo ambaye ndiye kipimo cha uhakika cha Ukristo.
8. **Jaribu kujiongeza:** Mtu anaweza kutumia muda mwingi na Mwislamu na wala isieleweke ni mada gani imezungumzwa na kumalizwa. Jaribu kuanzisha mada, na kamwe usijibu tu maswali yasiyohusiana na mada husika katika mazungumzo yenu.
9. **Mshirikishe kwa uchache:** Kama vile msemo usemao, "mwalimu mzuri hafundishi kila kitu anachojua; badala yake anajua anachofundisha." Mshirikishe kile unachojua kwa sehemu na kwa wakati maalum; Mwislamu anahitaji muda kufikiri juu ya yote unayojadiliana naye.
10. **Fanya maombi kuwa ndiyo silaha yako kuu:** Hii ni vita kati ya uzima na kifo, nuru na giza, Mungu na Shetani. Siyo hoja zetu za mabishano, bali ni Roho Mtakatifu ambaye atawashawishi Waislamu kuona haja ya kumkubali Yesu kuwa Mwokozi wa maisha yao.

# NENDA! HABARI ZA KANISA LA AFRIKA LINALOHAMASISHA WATU KWENDA

## BIBLIA YA KIARABU CHA KICHADI YACHAPISHWA

Biblia yote ya Kiarabu cha Kichadi imetafsiriwa na kuchapishwa kwa mara ya kwanza. Kupatikana kwa tafsiri hii ya Biblia kulisherehekewa hapo mwezi Aprili 2021 pamoja na matukio mawili ya kuwekwa wakfu katika mji mkuu wa Chad, N'djamena.

Zaidi ya Biblia 100 zilifika sehemu za Mashariki mwa nchi ya Chad mwezi Mei 2021, mahali ambapo timu ya SIM ipo. Shehena ya pili ya Biblia iliwasili mwezi Oktoba 2021. Mfanyakazi wa SIM, alinukuliwa akisema, "Sisi na wafanyakazi wenzetu ambao ni mmishenari hapa Chad tumefurahi sana kuwa na Biblia katika lugha ambayo watu wengi katika eneo hili la Dar Sila wanaielewa." Kiarabu cha Kichadi ni aina ya lugha zenye mchanganyiko na kifaransa na ndiyo lugha ya nchi na sehemu ya kusini mwa Chad ambayo wakazi wake wengi ni Waislamu.

Tafsiri ya Biblia hii imechukua zaidi ya miaka 20 kwa ushirikiano kati ya makanisa ya Chad, mashirika ya kimisheni ya Wycliffe na WE International. Mradi huu pia uliungwa mkono na jamii kubwa inayozungumza Kiarabu. Wachad pia wataweza kupata Biblia hii ya Kiarabu kupitia hata kwenye simu zao za mkononi zenye Tafadhali ombea usambazaji wa Biblia hizi katika nchi yote ya Chad, na hasa kwenye maeneo ambayo yana Waislamu wengi ambao kwa muda mrefu hapakuonekana uhitaji wa Biblia.

Kwa taarifa zaidi kuhusu tafadhali tembelea: https://bit.ly/3Iy3HY1.




## HABARI NA MAFUNZO

Kila mwezi Chuo cha umisheni cha Afrika Mashariki hutoa mafunzo ya umishenari kwa viongozi mbalimbali wa makanisa wakiwa ni wachungaji na wazee wa makanisa.

Viongozi hawa wa makanisa hufikiwa kupitia kiongozi mkuu wa makanisa ya sehemu maalumu makanisa yalipo kwa kuwa yeye huwafahamu viongozi wote na huwaleta viongozi hawa pamoja na kuwapa/kusambaza taarifa hiyo.

Mafunzo haya hufundishwa na Kelvin Mshema na viongozi wengine watatu, ambapo hufundisha mada 4 kwa muda wa siku 4 na mada zote na zipo kwa mtiririko kuanzia umisheni ulipoanzia na mpaka ulipo hivi sasa na mwisho wa siku wanajua kila kitu juu ya umisheni.



Lengo kuu la mafunzo hayo ya umisheni ni kwa lengo la kuwajuza watu na pia kupata watu wengine wanne watakaosimama katika nafasi nne muhimu za umisheni; muombaji, mtumaji, mhamasishaji na mutumwaji.

Wanapoanza mafunzo washiriki wote hupewa vitini vya somo husika la siku na kufuatilia kwa ukaribu kinachofundishwa kwa siku zote nne.

Wanapomaliza mafunzo hayo ya umisheni huwa kuna vitabu vinavyouzwa kwa bei nafuu sana kuwasaidia zaidi watu hawa waliohudhuria mafunzo.

## WASILIANA NA AFRITWENDE KUPITIA

Je, una maswali kuhusu somo hili au mada zingine kuhusu umisheni? Ni masuala gani ungependa AfriTWENDE ikuletee? Tunakaribisha mawazo yako, ili tuweze kuboresha jarida letu na liweze kutimiza lengo lake kwa ukamilifu iwezekanavyo. Tafadhali tuma baruapepe kwenda: afritwende@afrigo.org

Pia tunachapisha habari na taarifa za wamishenari sambamba na nukuu za kusisimua katika kurasa zetu mpya za mitandao ya kijamii. Tutembelee kwenye Facebook kwa www.facebook.com/afritwende na Instagram kwa www.instagram.com/afritwende. Pia unaweza kujipakulia taarifa zetu zote kwa tovuti ya www.afrigo.org/afri-twende.



# TAYARI KWA UJENZI WA TAIFA

NA KATE AZUMAH NA FURAHA KENGELA

Afisa mmoja kutoka Sekritarieti ya Jeshi la Kujenga Taifa alishindwa kubadilisha msimamo wa kuruta wawili. Kwa nini mtu ang'ang'anie kuwapeleka watumishi kwenye maeneo ya mbali vijijini wakati kuna nafasi bado kwenye maeneo ya mijini yenye huduma zote muhimu? Kuruta wengi wangekuwa tayari kulipa hata pesa kwa nafasi za mijini. Hata alifika mahali pa kufikiria kuwa vijana hao walikuwa ni wapelelezi.

Michael na Eben walikuwa sehemu ya msururu mrefu wa wa mishenari waliokuwa kwenye orodha ya Mkakati wa Tumikia Ulimwengu (OSG). Wakati wa majuma sita ya mafunzo kwa wa mishenari wakazi, walikuwa wakiiombea sana jamii ya Builsa.

## MKAKATI WA KUTUMIKIA ULIMWENGU

Mkakati huu (OSG) hufunza na kutuma vijana kama wamishenari kwenye jamii ambazo bado kufikiwa na injili wakati wanafanya wajibu wao wa Jeshi la kujenga taifa. Huko Ghana, kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa ni lazima kwa wote waliomaliza mafunzo ya vyuo vya kati na vyuo vikuu. Serikali huwapeleka maelfu yao kila mwaka kutumika katika sekta mbalimbali kama ajira za kitaifa na kuwalipa posho kila mwezi.

## MIRADI YA UFALME

"Kile ambacho Mungu amekirahisisha, sisi tusikifanye kuwa kigumu," anasema Mch. Sola Adebayo wa Miradi ya Ufalme wa Mungu unaoitwa The Kingdom Projects (TKP) nchini Nigeria. "Bwana hakusema, acha kazi yako na nenda ulimwenguni." Alichosema, ni kwamba, "Nendeni ulimwenguni kote na kuihubiri Injili."

TKP imepata njia endelevu za kufunza wafanyakazi wanaolipwa na serikali kutumika kama wamissionari katika maeneo wanayopelekwa baada ya mafunzo ya kujenga taifa. Jamii iko tayari kuwapokea wamishenari wa namna hii, na kazi zao za serikali hufungua milango ambayo vinginevyo isingeweza kufunguka. Mbinu ya namna hii hupunguza mzigo wa kutafuta msaada binafsi.

Chuo cha TKP cha watengeneza mahema huunganisha mafunzo ya umisheni kwa wale ambao huunganisha pamoja na kazi za serikali. Wamishenari waliofunzwa na TKP wamethibitika kuwa bora katika uinjilisti, ufundishaji wanafunzi na upandaji makanisa, uhamisishaji umisheni, umisheni wa matibabu ya binadamu, na shughuli za maendeleo ya jamii.

## MWALIMU AMBAYE NI MMISHENARI NCHINI TANZANIA

Iman ni mmishenari kutoka kijiji cha Mzenga wilaya ya Kisarawe Mkoani Pwani, ni mzawa wa eneo hilo. Iman aliokoka mwaka 2011 na kuamua kwenda kufanya kazi kwa watu ambao bado hawajafikiwa na injili.

Mwanzoni kabisa watu wa kabila hili walikuwa wagumu kumpokea na kumpenda lakini baada ya kuwaonyesha faida ya kazi ambazo zinawaletea fedha na chakula wakaanza kumpenda na hapo ndipo akaanza kufanya nao miradi mbalimbali.

Kwenye Kijiji hiki Iman ameunda vikundi vinne vya kujifunza Biblia ambavyo hufundisha na kuzungumzia mambo yaliyo kwenye Biblia na kujibu maswali mbali mbali ambayo watu hujiuliza kuhusu Yesu na Mungu. Maswali kama "Je, Yesu ni Mungu au sio Mungu?"

Siku za wiki Iman huenda kwenye kazi ya ualimu na mida ya jioni huenda kwenye huguli za kilimo na ufugaji ambazo hufanya pamoja na wanavikundi mbali mbali wa kijijni hapo. Kabla kuanza shuguli Iman aliwonyesha msingi na umuhimu wa kumtanguliza Mungu na hivyo na alifanya hivi ili iwe kaiwada ya wanakikundi hawa kuzoea, ili wasipate kutegemea namna mbadala au miungu mbadala katika shugh uli zao.

Iman anasema hakuna changamoto yeyote ile kwa upande wa kazi yake ya serikalini endapo tu atatimiza wajibu wake wa kazi anazotakiwa kufanya.

Iman na mke wake walifunga ndoa mwaka jana (2022). Mungu alimpatia mtu sahihi ambaye anafanya nae huduma kwenye eneo hili. Hivi sasa wamebarikiwa kupata mtoto mmoja mwaka huu, lakini pia wanaishi na mama yake mzazi Iman ambae ana changamoto za kiafya kidogo hivyo yupo hapo wakimuhudumia




Iman anasema umishenari hapo Mzenga unahitaji wito kutoka ndani na msaada wa Mungu. Mtu yeyote kwenye huduma kama hii anahitaji ajisimamamie mwenyewe, kuipenda huduma, bila kusahau kutilia mkazo kwenye kusoma neno na maombi.

www.afrigo.org/afritwende



# MAKUNDI YA WATU WAMATUMBI

Wamatumbi wapo takribani 250,000 na wanajulikana kama watu wa milimani. Milima hii hua ni ngumu kufikika, haswa msimu wa mvua na wengi wao huishi kwenye misitu. Haswa ni wakulima wa kujikimu, huvuna mpunga na kufuga kuku. Baadhi ya Wamatumbi wanaishi katika eneo linaloenda hadi kwenye bahari ya Hindi na Visiwa vya Songosongo na wao ni wavuvi. Baadhi ni wamiliki wa maduka madogo yaliyopo pembezoni mwa barabara kuu. Wanafuata mfumo dume na ndoa za mitala, ingawa talaka ni jambo la kawaida sana.

Wamatumbi ni watu huru na wanaojivunia, waaminifu, ingawa wana kipato cha chini na hawana ushawishi nchini Tanzania. Vijana wengi wanaweza kusoma na kuandika kiswahili, lakini kuna kiwango kikubwa cha kutojua kusoma na kuandika miongoni mwa wazee, ambao hutumia lugha ya kimatumbi zaidi. Wastani wa elimu huishia darasa la saba

Wamatumbi ni Waislamu kwa 99%, na hufanya sherehe na kutoa dhabihu kwa mapepo/mizimu. Kuna kuenea kwa matumizi ya uchawi na hirizi vile vile. Kazi ya umisionari inaendelea miongoni mwao, kwa njia mbalimbali kwa makanisa madogo ya kidhehebu yaliyo sambaa maeneo mbalimbali. Wamatumbi si wapingaji wa Injili lakini inaweza kuwa vigumu sana kwao kumwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Wale wanaomfuata Kristo wamekumbana na mateso fulani ambayo kwa ujumla hupungua baada ya muda fulani.

Kwa sasa kuna rekodi za Injili katika lugha yao, pamoja na hadithi za Biblia za mfuatano wa kimatukio iliyowekwa katika namna ya sauti, na filamu ya Yesu inapatikana pia. Injili na Matendo ya Mitume ni vitabu vilivyotafsiriwa katika lugha ya kimatumbi, na sehemu nyingine za Agano Jipya zinaendelea kutafsiriwa.

## Kwa muhtasari

- Kuanzia 1904-1908, Wamatumbi waliinuka kuupinga ukoloni wa Wajerumani nchini Tanzania.
- Wana pango kubwa liitwalo Nangoma, ambalo linaheshimiwa kama makazi ya mungu muhimu anayehusishwa na kucheza na kuabudu.
- Wanaume na wanawake wanashiriki majukumu ya kilimo kwa kushirikiana.

## Mahitaji ya kuombea

- Mungu awainue Wamatumbi ambao watahusika katika kuchochea vuguvugu la wanafunzi ambalo litaenea kwa wingi na zaidi.
- Wamishenari wa kigeni na wamishenari wa kitanzania, kwa ajili ya huduma yenye matunda.
- Wamatumbi watambue Yesu ni nani—Mwokozi wa karibu na wa kibinafsi, anayewapenda na mahitaji yao ya kila siku.


SIM By Prayer — AFRICA INLAND MISSION

**AFRITWENDE**: afritwende@afrigo.org **AFRIGO**: info@afrigo.org **ALLONS-Y !** : info@afrigo.org **AFRÍDE** : afride@afrigo.org

| SIM East Africa | SIM West Africa | SIM Southern Africa | AIM International |
|---|---|---|---|
| Tel: +251 911 206 530 | Tel: +233 30 222 5225 | Tel: +27 21 7153200 | amc.io@aimint.org |
| east-africa.office@sim.org | wamo.personnel@sim.org | za.enquiries@sim.org | aimint.org/africanmobilization/ |